kurugenzi Mhandisi Mshamu Munde na kulia Mbunge wa

Habari Leo, uk. 4 Tarehe 04/12/20

# Wadau nchini wahimizwa kuwekeza sekta ya mifugo

**Na John Mhala, Arusha**

WADAU mbalimbali wametakiwa kuchangamkia fursa ya kuwekeza katika sekta ya mifugo, ikiwemo kuboresha uzalishaji wa mazao ya mifugo ikiwemo nyama, maziwa na ngozi.

Aidha, kukua kwa sayansi na teknolojia, kutaharakisha kuboresha sekta hiyo muhimu, ambayo katika mwaka wa fedha 2019/2020 ilichangia zaidi ya Sh bilioni 44.85.

Hayo yalisemwa jana jijini Arusha na Katibu Mkuu wa Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Profesa Elisante Ole Gabriel, wakati akizindua maabara za Wakala wa Vyuo vya Mafunzo ya Mifugo nchini (LITA) Kampasi ya Tengeru.

Maabara hizo mbili zimekarabatiwa na kuwekewa vifaa vya kisasa kwa ufadhili wa serikali ya Poland kwa kushirikiana na Serikali ya Tanzania, ambapo serikali hiyo iliwakilishwa na Balozi wake hapa nchini, Krzysztof Buzalski.

Balozi wa Poland nchini Tanzania, Krzysztof Buzalski, alisema nchi yake itaendelea kushirikiana na Tanzania ikiwemo kujengea uwezo LITA katika eneo la utafiti na maabara.

Mtendaji Mkuu wa LITA nchini, Dk Pius Mwambene alisema maabara hizo zitatumika kutoa mafunzo kwa wanafunzi ili waweze kufanya uchunguzi wa magonjwa ya mifugo nchini na kutoa tiba sahihi.

Majaliwa, who was unimpressed factories and create jobs.

The Guardian UK. Turche 04/12/2020

# 'Tanzania's milk consumption still low though production up'

By Guardian Reporter

PRODUCTION of milk in the country has increased from 2.7 billion to 3.01 billion litres while milk drinking is reported to be still low.

This was revealed on Wednesday this week by Prof Elisante ole Gabriel, the Permanent Secretary (Livestock) in the Ministry of Livestock and Fisheries during his inspection tour of Galaxy Food and Beverages Limited in Arusha Region.

He said more efforts were needed to mobilise people to drink milk to improve their health.

"The country's milk consumption is 8 million litres per day. According to UN Food and Agricultural Organisation (FAO) every person is supposed to drink 200 litres of milk per year but a Tanzanian drinks at least 54 litres per year, I call all Tanzanians to increase their milk consumption to improve their health," said Prof Gabriel.

He called on the private sector, especially those in the dairy industry to continue supporting the government by ensuring they add value to their products including their quality packaging.

He further said his Ministry was bent on improving livestock breeds to have better cows, including appropriate vaccination and dipping.

He also called on dairy factory owners in the country to ensure they attain milk production levels according to the factories' installed capacities saying it was unprofitable to have low milk production as opposed to its capacity as the government also stands to lose revenue from various levies.

Irfhan Virjee, Galaxy Food and Beverages Limited Managing Director told the PS that Tanzania was supposed to be the second country in dairy production in Africa as it was the second in the continent with a huge population of livestock.

He thanked the government for its efforts in improving the environment in the establishment of the factory and pledged that production will increase due to the availability of markets within and outside the country.

Scanned with CamScanner

Mtanzanzia Uk. 6, Tarehe 04/12/2020

# Unywaji maziwa utaongeza ufahamu kwa wanafunzi

Na FARAJA MASINDE

MAPEMA mwaka huu, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto (mstaafu), Ummy Mwalimu alizitaka shule zote za msingi na sekondari nchini kuanza kuweka mazingira wezeshi kwa wanafunzi kunywa maziwa shuleni kwa kufungua vibanda na migahawa ya maziwa.

Kwa mujibu wa Ummy, kuanzisha vibanda vya maziwa shuleni hasa shule za kutwa, kutasaidia wanafunzi kuboresha afya zao, lakini pia kutasaidia kupanua soko kwa bidhaa hiyo muhimu.

Utafiti wa Shirika la Afya Duniani (WHO) unaonesha kwamba kila mtu anatakiwa kunywa nusu lita ya maziwa sawa na lita 180 kwa mwaka lakini kwa sasa kila mtu anakunywa lita 40 kwa mwaka sawa na vijiko 10 vya chai kwa siku.

Katika hilo, Ummy aliitaka Taasisi ya Chakula na Lishe Tanzania kuharakisha Mwongozo sahihi wa uandaaji vyakula vya nyongeza kwa Watoto vyenye virutubishi ambao unaandaliwa na Taasi hiyo kwa ushirikiano na Chuo Kikuu cha Afya na Sayansi Shirikishi Muhimbili (MUHAS) kupitia ufadhili wa shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP).

Hii inamaana kwamba shule zinapaswa kuwapa wajasiriamali nafasi ya kufungua vibanda vya kuuza maziwa kwa ajili ya wanafunzi kupata virutubisho hivyo wawapo shuleni, huku akivitaka viwanda kuwa na uwezo wa kutengeneza maziwa yenye ujazo angalau ujazo wa Mils 100, ili kukidhi mahitaji ya gharama na ununuzi kwa kila mtoto.

Huu ni uamuzi wa kupongezwa kwa Serikali kwa kuona umuhimu wa uwepo wa huduma hii mashuleni kwani itakuwa na manufaa makubwa kwa wanafunzi kwamba takwimu mbalimbali zinaonyesha kuwa watoto ambao wanapata maziwa wananafasi kubwa ya kufanya vyema darasani tofauti na wale ambao hawapati huduma hiyo.

Ni wajibu sasa kwa mamlaka husika zikiwamo shule na wadau muhimu kuhakikisha kuwa mpango huu wa Serikali unatekelezwa kwenye kila shule nchini ili uweze kuleta matunda kwa wanafunzi ambayo itakuwa faida ya taifa la kesho.

Kwani iwapo kizazi cha sasa kitafanya vyema kwenye taaluma basi ni dalili njema ya kuwa na taifa lemnye watu kwenye uwezo mkubwa wa kufanya mambo.

Scanned with CamScanner

# Wataalmu wa mifugo watakiwa kutumia taaluma zao

Na Mbaraka Kambona, Dodoma

WATAALAMU wa Mifugo wametakiwa kutumia taaluma zao na kushiriki kikamilifu katika kubuni mbinu za kisasa za kuinua viwango vya minyororo ya thamani ya mazao ya Mifugo na Uvuvi ili kuleta tija na kukidhi mahitaji ya uchumi wa viwanda kwa maendeleo endelevu ya kijamii na kiuchumi.

Kaimu Katibu Mkuu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Amos Zephania alisema hayo alipokuwa akifungua Kongamano la 43 la Kisayansi la Uzalishaji na Uendelezaji wa Mifugo na Uvuvi na Mkutano wa 44 wa mwaka wa Chama cha Wataalamu wa Uzalishaji na Uendelezaji wa Mifugo Tanzania linalofanyika jijini Dodoma kuanzia Desemba 2- 4, 2020.

Zephania alisema kuwa Serikali imedhamiria kuanzisha na kuendeleza viwanda mbalimbali hususani vya uzalishaji na usindikaji wa mazao ya kilimo na mifugo ambavyo ni msingi wa maendeleo endelevu.

"Serikali inatambua kuwa maendeleo ya viwanda hapa nchini yatachagiza upatikanaji wa bidhaa muhimu na bora kwa matumizi ya ndani na nje ya nchi jambo ambalo litainua ubora na viwango vya maisha ya wananchi, kujenga uchumi imara na kukuza uchumi wa Taifa unaoweza kuhimili ushindani wa kikanda na kimataifa," alisema Zephania

Aliendelea kusema kuwa ni wazi kwamba mifumo ya uzalishaji wa mifugo na uvuvi katika nchi yetu imeegemea zaidi katika uzalishaji kwa mifumo ya asili ambapo wazalishaji wengi ni wafugaji na wavuvi wadogo wadogo.

Aliongeza kuwa mifugo mingi iliyopo bado ni ya asili ambayo tija katika uzalishaji wako haiiridhishi huku akisema kuwa ngómbe wengi wa asili wana uzito mdogo wa kati ya kilo 200 hadi 350 ambao hupelekea kutoa maziwa kidogo na nyama kidogo ambayo haizidi wastani wa kilo 175.

Kufuatia hali hiyo, Zephania alisema kuwa Wataalamu wa Mifugo wanajukumu la kufanya kuleta mabadiliko katika mifumo ili kuongeza ufanisi na tija ya uzalishaji kwa kutumia sayansi na teknolojia za kisasa huku akiwasisitiza kuwasaidia wafugaji waweze kuongeza ubora wa uzalishaji ili mali ghafi za uhakika ziweze kupatikana kwa matumizi ya viwanda vya kusindika mazao ya mifugo na uvuvi.

Aidha, Zephania aliwahimiza wataalamu hao kuendelea kuimarisha afya za mifugo, usimamizi wa mifumo bora ya uzalishaji na kutoa huduma za ugani kwa wakati sambamba na uboreshaji wa miundombinu ya masoko ikiwemo uhifadhi, usafirishaji na usambazaji wa mazao hayo huku akisema kuwa mazao ya mifugo na uvuvi yanaharibika upesi yasipotunzwa na kuhifadhiwa ipasavyo.

Naye, Katibu Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Maduka Kessy alisema kuwa jukumu la Wataalamu hao ni kuinua tija na faida kwa wafugaji wanaoshiriki katika uwekezaji kwenye mnyororo mzima wa thamani.

Kessy aliongeza kuwa Mkoa wa Dodoma una zaidi ya Kaya Mia nne na Hamsini Elfu (450,000) na kati ya kaya hizo Asilimia 44 ni wafugaji na ndio wenye kipato cha chini na maendeleo yao ni duni, hivyo kuna haja ya kuwaendeleza ili waweze kunufaika na mifugo yao.

"Dodoma ni miongoni mwa mikoa inayoongoza kwa kuwa na mifugo mingi, mpaka sasa takwimu zinaonesha tuna ng'ombe milioni 1.8 lakini mnyororo wa thamani kwa mifugo hiyo ni mfupi sana, hivyo kuwepo kwenu hapa leo ni faraja ya kwamba mtakuwa chachu ya mabadiliko kwa wafugaji wetu ili waweze kufaidika na mifugo yao," alisema Kessy

Kessy aliendelea kusema kuwa mfumo wa ufugaji kwa wananchi wengi umepitwa na wakati huku akiongeza kuwa kasi ya ukuaji wa mji wa Dodoma ni kubwa hivyo kuna haja ya kutafuta namna ya kuchangamanisha ukuaji wa mji na maendeleo ya sekta ya mifugo.

**Asilimia 65 >> Ni chanzo kikuu cha ajira ya nguvu kazi nchini**

# Kilimo, mifugo, uvuvi kinara pato la Taifa

**Mwanza**

**Na PETER KATULANDA**

SENSA ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka 2019/2020 imebainisha kuwa sekta hiyo inachangia pato la taifa kwa wastani wa asilimia 27.5.

Kwa mujibu wa sensa hiyo, sekta hiyo inaingiza fedha za kigeni asilimia 24.7 na ni chanzo kikuu cha ajira kwa kuajiri zaidi ya asilimia 65 ya nguvu kazi nchini.

Sensa hiyo ya tano tangu Tanzania ipate Uhuru mwaka 1961 imebainisha uzalishaji wa mahindi umeongezeka kwa asilimia 4.1, mpunga asilimia 100 na mtama ukishuka asilimia 11.5 tangu Sensa ya kilimo, mifugo na uvuvi ya mwaka 2007/2008.

Sensa hiyo imeonyesha Tanzania inaendelea kuwa nchi ya pili Afrika kwa kuwa na ng'ombe 33,943,183 nyuma ya Ethiopia yenye ng'ombe milioni 60.39.

Akitangaza matokeo ya awali ya Sensa hiyo jijini hapa, Mtakwimu Mkuu wa Serikali wa Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Dk. Albina Chuwa alisema matokeo ya awali yanaonesha kaya milioni 7.8 (sawa na asimilia 65.3) zinajihusisha na kilimo.

"Kati ya kaya hizo, milioni 7.7 kutoka Tanzania Bara na 180,219 Zanzibar na asilimia 65 ya kaya hizo, zinajihusisha na shughuli za kilimo cha mazao na asilimia 33 mazao na mifugo, asilimia mbili ufugaji," alisema Dk. Chuwa.

Sensa hiyo imeonesha tani milioni 9.1 za mazao makuu ya chakula kwa nafaka (mahindi, mpunga na mtama) zilizalishwa msimu wa kilimo wa mwaka 2019/2020.

Mahindi yalikuwa tani milioni 5.7 sawa na asilimia 62.5 ya nafaka, ikifuatiwa na mpunga tani milioni 2.9 sawa na asilimia 32.1, mtama tani 488,724 sawa na asilimia 5.4.

Kwa mazao makuu ya biashara, kahawa iliyozalishwa ilikuwa tani 92,396, chai tani 40,611, pamba tani 445,972 na karafuu tani 3,378.

Matokeo ya Sensa hiyo yanaonesha kuwa, hekta milioni 13.5 zililimwa mazao mbalimbali, kati ya hizo, asilimia 76.7 zilitumia mbegu za asili, asilimia 20.8 zilitumia mbegu bora, na asilimia 2.5 zilitumia mbegu za aina zote mbili.

Katika mwaka wa kilimo 2019/20, hekta milioni 2.8 zilitumia mbolea, kati ya hekta hizo, asilimia 60.7 zilitumia mbolea za asili na asilimia 39.3 zilitumia mbolea za viwandani.

Matokeo ya sensa hiyo yanaonesha kaya za wakulima wadogo zilisindika mazao yao ili kuongezea thamani kwa ajili ya soko. Mazao yaliyosindikwa kwa wingi ni mahindi (tani 706,464), mpunga (tani 193,462) na alizeti (tani 113,289).

Dk. Chuwa alisema sensa hiyo ya Tano ya mwaka 2019/2020 imetumia sh. bilioni tano na kuokoa sh. bilioni tano ambazo ni sawa na nusu ya fedha zilizotumika wakati wa sensa ya nne ya mwaka 2007/2009.

Kazi hiyo imefanyika kwa teknolojia ya kidijitali na kutumia kipindi cha miezi miwili toka Agosti 5/2020 na kukamilika Oktoba 2/2020.

Scanned with CamScanner

ilizochukuliwa Kinondoni kama mkopo

# esha mikopo ni kukiona

i wapo kwenye matanga, ye matanga tutawarejesha i kurejesha," alisema.

alisema kiasi ambacho mefikia zaidi ya sh. bilioni hauri hiyo, jambo alilosema

watu wanategemea ziwatoe hiyo yeyote aliyechukua, a," alionya Chongolo.

wajasiriamali hususan wadogo, kuchangamkia na na fedha hizo badala ya aka kukosa mitaji.

za ni kwamba, wajasiriamali a kelele ya mitaji na sisi tuna zaidi ya sh. bilioni tunazotenga kwa ajili ya mikopo hiyo," alisema.

Alisema sh. bilioni tatu ni fedha nyingi ambapo kwa wanawake wanapata asilimia 4.0 sawa na zaidi ya sh. bilioni 1.0 , vijana wanapata asilimia 4.0 sawa na zaidi ya sh. bilioni 1.0 na watu wenye ulemavu wanapata asilimia 2.0 sawa na zaidi ya sh. milioni 500.

Aliwataka wafanyabiashara na wajasiriamali kujiepusha na fedha wanazokopa mitaani zinazofahamika kama mikopo umiza.

"Watu wanakopa laki moja riba ni elfu thelathini, hiyo ni fedha nyingi na wapo wajanja wachache wanaojinufaisha na mikopo hii umiza, msiende huko njooni halmashauri mpate fedha zisizo na riba, ukikopa milioni moja unarejesha milioni moja," alisema.



a Mama na Mtoto katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa ya

## ra waongeze ubunifu wa biashara

kufanya biashara, moja Rais Dk. John igozo wa dhamira ya

aya wafanyabiashara alieleza.

wi karibuni ambapo wa wafanyabiashara nchini humo, lakini angazwa kikamilifu. pekee.

tu wafanyabiashara TRA kwa kutokea a nyuma, jambo taifa uendana na a Gabona.

Rais Dk. Magufuli chumi wa kati, ni u wenye ubunifu katika wafanyabiashara wenye diplomasia, tunafanya makosa kutoshirikisha viongozi, ni muhimu tutumie mabaraza ya wilaya kujenga diplomasia ya biashara hasa unapokwenda nje ya nchi."

Kwa upande wake, Ofisa Biashara na Masoko ya Nje wa Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (TanTrade) Tito Norris, alisema serikali iko katika michakato mbalimbai kuhakikisha inaboresha mazingira kwenye sekta hiyo kupitia mifumo mbalimbali ikiwemo Blue Print.

"Lengo ni kupunguza gharama za maisha kwa wafanyabiashara. Pia kuwasaidia wafanyabiashara kuboresha na kukuza biashara kisha serikali kupata mapato," alisema.

Alieleza kuwa maofisa biashara katika manispaa, ni wawezeshaji wa biashara kwa mujibu wa sera na jukumu lao ni kuwasaidia kuboresha biashara na

# Uzalishaji maziwa nchini waongezeka

Dodoma

Na FRED ALFRED

UZALISHAJI wa maziwa nchini umeongezeka kutoka lita bilioni 2.7 kwa mwaka hadi lita bilioni 3.01.

Hata hivyo, licha ya uzalishaji wa bidhaa hiyo kuongezeka, matumizi ya maziwa hapa nchini, bado yako chini.

Hayo yalisemwa jana na Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo), Profesa Elisante Gabriel, alipotembelea Kiwanda cha Galaxy Food and Beverages Limited kilichopo mkoani Arusha.

Lengo la ziara hiyo ilikuwa ni kujionea namna viwanda vya maziwa vinavyozingatia ubora wa bidhaa wanazozalisha.

Profesa Gabriel alisema jitihada zaidi zinatakiwa kuwahamasisha wananchi kunywa maziwa ili kuboresha afya zao.

"Matumizi ya maziwa nchini ni lita milioni nane kwa siku, ambapo kwa mujibu wa Shirika la Chakula na Kilimo Duniani (FAO), kila mtu anatakiwa kunywa lita 200 za maziwa kwa mwaka, lakini kwa Tanzania unywaji wa maziwa kwa mtu umefikia walau lita 54 kwa mwaka," alisema.

Profesa Gabriel alitoa wito kwa

> **"Wenye viwanda vya maziwa nchini, mnatakiwa kuzalisha bidhaa bora ili Watanzania wawe na imani na viwanda vyenu na kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kwani kwa kufanya hivyo ajira zitaongezeka sambamba na mapato ya serikali.**
>
> Profesa Elisante Gabriel
> Katibu Mkuu Wizara ya Mifugo na Uvuvi (Mifugo)

sekta binafsi hususan waliopo kwenye tasnia ya maziwa nchini, kuendelea kuiunga mkono serikali kwa kuhakikisha wanaongeza thamani ya bidhaa zao pamoja na kuziweka kwenye vifungashio tofauti kulingana na mahitaji ya wateja wao.

Pia aliwitaka viwanda vya maziwa nchini kuhakikisha vinafikia uwezo wa kiwanda uliosimikwa katika uzalishaji wa maziwa kwa kuwa ni hasara kuzalisha kidogo tofauti na uwezo wake kwani kwa kufanya hivyo wenye viwanda wanapata hasara na pia serikali itapata mapato kidogo kutokana na tozo mbalimbali.

"Wenye viwanda vya maziwa nchini, mnatakiwa kuzalisha bidhaa bora ili Watanzania wawe na imani na viwanda vyenu na kutumia bidhaa zinazozalishwa nchini kwani kwa kufanya hivyo ajira zitaongezeka sambamba na mapato ya serikali," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Kiwanda cha Galaxy Food and Beverages Limited, Irfhan Virjee, alisema Tanzania inatakiwa iwe nchi ya pili kwa kuzalisha maziwa mengi na kusambaza katika nchi mbalimbali, kwa kuwa ni ya pili barani Afrika kwa kuwa na mifugo mingi na kwamba soko la maziwa bado ni kubwa.

"Tunaishukuru serikali kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa kuwa kiwanda hiki kimeanzishwa katika serikali ya awamu ya tano," alisema.

Alisema uzalishaji utazidi kuongezeka kutokana na uwepo wa masoko kutoka ndani na nje ya nchi.

Scanned with CamScanner